

OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
SHULE YA SEKONDARI KIRETI, S.L.P. 313 LUSHOTO

JINA LA MWANAFUNZI □ □ □ □

FOMU YA MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Kwa niaba ya walimu wa shule ya sekondari Kireti ninayo furaha ya kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Kreti ambayo ni shule ya Kutwa.

Wewe ni miongoni mwa vijana wachache waliopata bahati hii adimu hivyo ni matumaini yetu kuwa utaitumia nafasi hii ipasavyo ili baadae ulisaidie Taifa lako.

Pia nimatumaini yetu kuwa utakuwa na bidii katika masomo na shughuli nyingine shuleni na hata kwenye jamii inayokuzunguka.

Ninapenda pia kukutaarifu kuwa shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 Saa 1:00 Asubuhi, hivyo unapaswa kuripoti shuleni tarehe tajwa bila kukosa ukiwa na mzazi wako.

ORODHA YA MAHITAJI YA SHULE

A. SARE ZA SHULE

Wasichana

- i. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunga kwa kamba visiwe raba
- ii. Soksi nyeupe jozi mbili
- iii. Mashati meupe mawili ya mikono mifupi
- iv. Sketi mbili za rangi ya damu yam zee kitambaa kiwe namba moja (zingatia sana kitambaa ulichopewa)
- v. Sweta la rangi ya kijani.
- vi.

NB:

Kwa ajili ya wasichana wa kiislamu watakaopenda kuvaa hijabu na suruali zisizobana wanaruhusiwa

Wavulana

- i. Viatu vyeusi visigino vifupi vya kufunga kwa kamba visiwe raba
- ii. Soksi nyeusi jozi mbili
- iii. Mashati meupe mawili ya mikono mifupi
- iv. Suruali mbili za rangi nyeusi kitambaa kiwe namba moja (zingatia sana kitambaa ulichopewa)
- v. Sweta moja la shule la rangi ya kijani

B. VIFAA VYA TAALUMA

- ✓ Kalamu za wino za kutosha na penseli
- ✓ Daftari kubwa kumi (10) quire three
- ✓ Daftari ndogo kumi (10) kwa ajili ya mitihani ya wiki kwa kila somo
- ✓ Mkebe (mathematical set)
- ✓ Begi la kubebea daftari
- ✓ Kamusi ya kiingereza (dictationary)

NB: Fomu ya hospitali ijazwe na daktari wa hospitali ya serikali, na siku ya kuripoti mwanafunzi aje na fomu zote zikiwa zimejazwa kikamilifu.

Nakutakia utekelezaji mwema

KARIBU SANA KIRETI SEKONDARI

CHARLES D. NYANGALIMA
MKUU WA SHULE

SHERIA ZA SHULE

Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule.

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- i) Kuoja au kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

OR-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Shule ya Sekondari Kreti S.L.P 313, Lushoto.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI

Ahadi ya Mzazi na Mwanafunzi kukiri na kukubali Sheria, Kanuni, Taratibu na Kutii Maagizo Halali ya shule.

A. IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWWE

1. Majina kamili _____
2. Tarehe ya kuzaliwa _____
3. Dhehebu _____
4. Mahali alipozaliwa _____ Wilaya _____

Nimesoma maagizo yote ya kujiunga na Shule ya Sekondari □□□□□□□..
na nimekubali kutimiza masharti na sheria zote za shule.

SAINI YA MWANAFUNZI □□□□□□□... **TAREHE** □□□□□□□□

B. IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWWE

1. Majina kamili _____
2. Wewe ni Mzazi (**NDIYO/HAPANA**) Mlezi (**NDIYO/HAPANA**) kata isiyohusika.
3. Kazi yako ni _____
4. Anuani ya nyumbani/kazini/ yoyote ya karibu _____
5. Namba ya simu _____

Mimi Mzazi/Mlezi nimesoma maelezo yote na kuyaelewa vizuri. Nitakuwa tayari kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi Shuleni na nyumbani. Pia nipo tayari kumlipia mwanangu chakula cha mchana awapo shuleni. Niko tayari kuchukuliwa hatua za kisheria pale mwanangu atakapotoroka shule au kuacha shule pasipo kumfuatilia.

SAINI YA MZAZI/MLEZI □□□□□□□□□□□□.. **TAREHE** □□□□□□□□□□

